



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26-2963822
Nukushi: +255 26-2963828
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma
TANZANIA.



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb Na: NBS/S.40/21/541

YALIYOJITOKEZA

Tarehe: 08 Oktoba, 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI SEPTEMBER, 2018

MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma 278 zikiwa ni pamoja na bidhaa 97 za Vyakula na Vinywaji Baridi na 181 zisizo za Vyakula hukusanywa kila mwezi katika kila mkoa.

Mizania za Bidhaa na Huduma za Jamii na Kizio cha Bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijiji yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2011/12. Kizio cha bei kinachotumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Desemba, 2015.

Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa hufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi za Bei zinajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa nyumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za Bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi za mwanzo hukokotolewa kwa kutumia wastani wa jiometria "geometric mean of Price Relatives". Kanuni ya Lowe Index Formula ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" hutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZeka KIDOGO HADI ASILIMIA 3.4

Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Septemba, 2018

(Des. 2015 = 100)

Na. .	KUNDI (MAIN GROUP)	Mizania (Weight)	Sept-17	Agosti- 18	Sept-18	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na vinywaji baridi	38.5	112.40	115.34	114.65	-0.6	2.0
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.7	107.15	108.40	109.22	0.8	1.9
3	Mavazi ya nguo na viatu	8.3	106.34	109.29	109.71	0.4	3.2
4	Nishati, Maji na Makazi	11.6	118.38	131.20	133.95	2.1	13.1
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.3	104.80	107.91	107.90	0.0	3.0
6	Gharama za Afya	2.9	106.19	108.01	107.55	-0.4	1.3
7	Usafirishaji	12.5	99.57	102.70	102.38	-0.3	2.8
8	Mawasiliano	5.6	98.10	95.50	95.57	0.1	-2.6
9	Utamaduni na Burudani	1.6	103.07	102.66	102.88	0.2	-0.2
10	Elimu	1.5	103.43	105.99	105.99	0.0	2.5
11	Hoteli na Migahawa	4.2	104.37	105.55	106.32	0.7	1.9
12	Bidhaa na huduma nyinginezo	3.1	105.67	106.91	107.05	0.1	1.3
JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE		100.00	108.48	112.01	112.12	0.1	3.4

Makundi Mengine Teule

1	Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na mahotelini	37.1	113.37	117.47	116.84	-0.5	3.1
2	Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli	8.7	122.34	142.51	145.44	2.1	18.9
3	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula	62.9	106.26	110.81	111.38	0.5	4.8
4	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, nishati na mafuta	54.3	103.68	105.74	105.93	0.2	2.2

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2018 umeongezeka kidogo hadi asilimia 3.4 kutoka asilimia 3.3 kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2018. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2018 imeongezeka kidogo ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2018. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 112.12 mwezi Septemba, 2018 kutoka 108.48 mwezi Septemba, 2017.

Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Septemba, 2018 umeendelea umepungua hadi asilimia 2.0 kutoka asilimia 2.2 ilivyokuwa mwezi Agosti, 2018. Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwaka kwa bidhaa za vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani kwa mwezi Septemba, 2018 umepungua pia hadi asilimia 3.1 kutoka asilimia 3.2 mwezi Agosti, 2018. Aidha, badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula kwa mwezi Septemba, 2018 limeongezeka hadi asilimia 4.8 kutoka asilimia 4.6 mwezi Agosti, 2018.

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma zote isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Septemba, 2018 umeongezeka hadi asilimia 2.2 kutoka asilimia 2.0 mwezi Agosti, 2018.

Fahirisi inayotumika kukokotoa aina hii ya Mfumuko wa Bei, hajumuishi vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa, kuni na umeme. Vyakula na bidhaa za nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara, hivyo vikiondolewa kwenye fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Septemba, 2017 hadi Septemba, 2018. (Des. 2015 = 100)



Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Septemba, 2017 hadi mwezi Septemba, 2018. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei umekuwa kati ya asilimia 5.3 mwezi Septemba, 2017 na asilimia 3.3 kwa mwezi Agosti, 2018.

MABADILIKO YA FAHIRISI ZA BEI KATI YA MWEZI AGOSTI, 2018 NA MWEZI SEPTEMBA, 2018.

Badiliko la Fahirisi za Bei kati ya mwezi Agosti, 2018 na mwezi Septemba, 2018 limeongezeka kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na badiliko la kupungua kwa asilimia 0.4 mwezi Agosti, 2018 kutoka mwezi Julai, 2018. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 112.12 mwezi Septemba, 2018 kutoka 112.01 mwezi Agosti, 2018. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na; mavazi ya wanaume kwa asilimia 4.2, viatu vya wanawake kwa asilimia 2.9, kodi ya pango kwa asilimia 2.4, vifaa vya matengenezo na ukarabati wa nyumba kwa asilimia 2.7, kuni kwa asilimia 6.8 na vitabu vya shule kwa asilimia 1.4.

Jedwali Namba 2: Shajala ya Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Oktoba, 2018	08 th Novemba, 2018
Novemba, 2018	10 th Desemba, 2018
Desemba, 2018	08 Januari, 2019

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma,
TANZANIA.

Simu: +255 26 -2963822

Nukushi: +255 26 -2963828

Barua pepe: dg@nbs.go.tz;

Tovuti: www.nbs.go.tz